


HABARI KITAIFA

LATRA yakumbushwa utekelezaji maagizo ya Rais

Na Mwandishi Wetu

KATIBU Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, ameitaka Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhi (LATRA), kuharakiisha utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la mfumo jumuishi wa mauzo ya tiketi unaofahamika kwa Safari Tiketi.

Akizungumza jana baada ya kutembelea Banda la LATRA kwenye Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, jijini Dar es Salaam, alisema ni muhimu kuhakikisha wamiliki wa mifumo ya tiketi mtandao nchini wanaunganisha mifumo yao.

Alisema jambu hilo ni la kisheria na kikanuni ambalo ni lazima kufuatwa ili kuhakikisha serikali inapata mapato yake kikamilifu.

"Nakumbuka Rais Samia alipokuwa akizindua treni ya kisasa pale Dodoma, alitoa maelekezo manane na mojawapo ni hili la kuwa na mfumo jumuishi wa tiketi mtandao.

"Tunafurahi kwamba LATRA wameliwezesha hili

na mfumo huu unamwezesha abiria kukata tiketi za mabasi pamoja na treni za kisasa (SGR) na za reli ya kati (MGR) kwa urahisi kwa njia ya mtandao," alisema Prof. Kahyarara.

Aidha, alisema mfumo wa safari tiketi unasaidia wamiliki wa mabasi kupata mapato yao papo hapo na pia unarahisisha ufuatiliaji wa mabasi yanayotoa huduma pamoja na kufahamu idadi ya abiria wanaosafiri.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu Suluo, alisema ni kosa kisheria kuwa na mfumo wa kutoa tiketi mtandao bila kuthibitishwa na LATRA.

Aliwataka wamiliki wa mabasi kutotumia kampuni za tiketi mtandao zisizoidhinishwa na LATRA baada ya Julai 14, mwaka huu.

"Wamiliki nawatahadharisha msije mkaingia



Nakumbuka Rais Samia alipokuwa akizindua treni ya kisasa pale Dodoma, alitoa maelekezo manane na mojawapo ni hili la kuwa na mfumo jumuishi wa tiketi mtandao.

kwenye matatizo ya kuzuiliwa kutoa huduma kwa kuwa usipotoa tiketi mtandao, huruhusiwi kufanya kazi ya usafirishaji na pia huruhusiwi kupata leseni.

"Tumewapa taarifa za awali kuhusu kampuni ambazo hazijakamilisha utaratibu kwa hiyo muwafuatilie na mhakikishe mnamumia kampuni zilizokidhi vigezo mara baada ya muda waliopewa kuisha," alisisitiza CPA Suluo.

Julai 2, mwaka huu LATRA ilitangaza kampuni tatu za tiketi mtandao ambazo mifumo yao imekidhi vigezo.

Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhi za mwaka 2024 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la Januari 12, 2024 zimeweka vigezo vya kupata kibali ambavyo ni pamoja na mfumo husika kuwa na ulinzi dhidi ya uvamizi wa kimtandao na kuwa na uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya serikali.

Govt wants Latra to enforce e-ticketing integration drive

By Getrude Mbago

THE government has directed the Land Transport Regulatory Authority (LATRA) to ensure that all owners of digital ticketing platforms in Tanzania integrate their systems with the government's unified ticketing system, 'safari tiketi', in accordance with existing laws and regulations.

Speaking during a visit to LATRA's pavilion over the weekend at the 49th Dar es Salaam Interna-

tional Trade Fair (DITF) on July 5, Prof. Kahyarara said this directive is in line with President Samia Suluhu Hassan's instruction to enhance transparency and efficiency in the country's public transport services.

"I recall that when President Samia launched the modern train service in Dodoma, she issued eight directives—one of which was the implementation of a unified e-ticketing system. We commend LATRA for making this a reality. The 'safari

tiketi' system enables passengers to book bus and train tickets online, seamlessly," Prof. Kahyarara said.

He added that the system supports bus operators by providing instant revenue collection and real-time tracking of passenger volumes and vehicle operations, improving oversight and service delivery.

LATRA director general, CPA Habibu Suluo issued a stern warning to bus operators against using unregistered e-ticketing companies. He stated that from July 14, 2025, it

will be unlawful to operate without LATRA-approved e-ticketing systems.

"Operators must ensure they do not work with unapproved ticketing platforms. After July 14, any company found in violation will be prohibited from operating. LATRA will also withhold transport licences from any non-compliant operator," Suluo said.

As of July 2, 2025, LATRA approved three e-ticketing companies: Otapp Agency Company Lim-

ited, Hashtech Tanzania Limited, and Iyishe Company Limited. An additional six companies, AB Courier Express Ltd, Busbora Company Ltd, Logix Company Ltd, Mkombozi Infotech Company, Sepatech Company Ltd, and Web Corporation Ltd, were given 14 days to address technical challenges before final approval.

Two other companies, Duarani Innovative Company and Itule Company – were flagged for major compliance issues and have been

given a 7-day grace period. If they fail to meet the required standards, they will be barred from offering e-ticketing services, and their clients will be advised to migrate to approved providers.

According to Regulation 5 of the 2024 LATRA Online Ticketing Regulations, published in Government Gazette No. 20 of January 12, 2024, any e-ticketing system must include cyber-security protections and be technically compatible with government infrastructure.

Jamhuri Jumanne Julai 8, 2025 Pg 4



Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Profesa Gadius Kahyarara (katikati) akiagana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) baada ya kutembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) jijini Dar es Salaam.